TAARIFA YA MAELEZO YA CHANJO SWAHILI

# Chanjo ya homa ya Uti wa Mgongo (Meningococus) ACWY: Unachohitaji kujua

**Many Vaccine Information Statements are available in Spanish and other languages. See www.immunize.org/vis**

**Hojas de información sobre vacunas están disponibles en español y en muchos otros idiomas. Visite www.immunize.org/vis**

## 1 Ni kwa nini unapaswa kuchanjwa?

Ugonjwa wa homa ya **Uti wa mgongo (meningitis)** ni ugonjwa hatari unaosababishwa na aina ya bakteria inayoitwa *Neisseria meningitidis*. Bakteria hii husababisha homa ya uti wa mgongo (ugonjwa wa ubongo na uti wa mgongo) na maradhi ya damu. Ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo mara nyingi hutokea bila onyo hata kwa watu walio na afya bora.

Ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo yaani meningitis unaweza kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mtu mwingine kwa kuguzana kwa karibu kama vile kukohoa au kubusiana, na pia kwa mguzo wa mbali, hasa kati ya watu wanaoishi nyumba moja.

Kuna makundi 12 ya bakteria za Neisseria meningitidis Makundi haya ya bakteri ya A, B, C, W, na Y husababisha ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo.

Mtu yeyote anaweza kuupata ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo lakini kuna aina ya watu fulani ambao wamo katika hatari kubwa ya kuambukizwa. Watu hawa ni kama vile:

- Watoto wachanga walio chini ya umri wa mwaka mmoja
- Vijana wachanga wenye umri kati ya miaka 16 hadi miaka 23
- Watu walio na ugonjwa fulani ambao matibabu yake yanaweza kuathiri mfumo wa kinga mwilini
- Wataalamu wa mikrobiolojia wanaofanya kazi na chembechembe za *N. meningitidis*
- Watu walio katika maeneo hatari ya janga la kuzuka kwa ugonjwa katika jamii

Hata kama ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo unatibiwa, ugonjwa huu huua kati ya watu 10 hadi 15 kati ya watu 100 ya wale walioathiriwa na ugonjwa huu Takriban watu 10 hadi 20 kati ya 100 ya wale wanaopona wataugua ulemavu kama vile kupoteza uwezo wa kusikia, matatizo ya ubongo, matatizo ya figo, kukatwa viungo, matatizo ya mfumo wa neva, au kovu kutokana na upasuaji wa ngozi.

Chanjo ya Homa ya Uti wa **Mgongo ACWY inasaidia** kupunguza ugonjwa unaoletwa na viini vya makundi A, C, W, na Y. Kuna chanjo nyingine ya Homa ya Uti wa Mgongo inayosaidia kukinga bakteria ya kundi B.

## 2 Chanjo za Homa ya Uti wa Mgongo ACWY

Chanjo ya homa ya Uti wa mgongo (MenACWY) imeidhinishwa na idara ya Usimamizi wa Chakula na Madawa (FDA) ili kusaidia kuzuia magonjwa ya homa ya uti wa mgongo yanayosababishwa na makundi ya bakteria ya A, C, W, na Y.

Dozi mbili za MenACWY hupendekezwa mara kwa mara kwa vijana wenye umri wa miaka 11 hadi miaka 18. Dozi ya kwanza hupeanwa kati ya umri wa miaka 11 au 12, na dozi ya pili katika umri wa miaka 16. Baadhi ya vijana, pamoja na wenye ugonjwa wa UKIMWI, wanafaa kupokea dozi za ziada. Muulize mtoa huduma wako akupe maelezo zaidi kuhusu idadi na marudio ya dozi na mahitaji ya dozi za nyongeza.

Bali na chanjo za kawaida kwa vijana, chanjo ya MenACWY pia hupendekezwa kwa makundi fulani ya watu kama vile:

- Watu walio hatarini kwa sababu ya kuzuka kwa ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo ya makundi ya bakteria ya A, C, W, au Y
- Watu walio na Ukimwi
- Mtu yeyote ambaye wengu wake umeharibika au umetolewa, pia wagonjwa wa sikoseli
- Mtu mwenye ugonjwa nadra unaoathiri mfumo wa kinga mwilini unaoitwa "upungufu na endelevu wa vijenzi saidizi"
- Mtu yeyote anayetumia dawa inayoitwa *eculizumab* (pia *inaitwa Soliris*®)
- Wataalamu wa mikrobiolojia wanaofanya kazi na watu wenye chembechembe za *N. meningitidis*
- Mtu yeyote anayesafiri ama anayeishi katika maeneo ya dunia ambapo ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo hutokea mara kwa mara, kama vile sehemu za Afrika
- Wanafunzi wapya kwenye vyuo vikuu wanaoishi katika mabweni
- Makurutu wa jeshi la Marekani

Watu walio na hali fulani za kimatibabu wanahitaji dozi kadhaa kwa kinga ya kutosha. Muulize mtoa huduma wako wa afya kuhusu idadi na marudio ya dozi na mahitaji ya dozi za nyongeza.

## 3 Baadhi ya watu hawafai kupokea chanjo hii

Unastahili kumjulishe mtu anayekupa chanjo kama Una mizio *(Alaji)* yoyote hatari ya kutishia Maisha yako. Ikiwa umewahi kuwa na mzio wa kutishia maisha baada kupata dozi ya chanjo ya homa ya uti wa mgongo (ACWY) hapo awali, au ikiwa wewe hupata mzio mkali *(Alaji)* katika sehemu yoyote ya chanjo hii, hufai kupokea chanjo hii. Mtoa huduma wako anaweza kukupa maelezo zaidi kuhusu viungo vya chanjo hii.

U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

Hakuna maelezo mengi kuhusu hatari zinazotarajiwa za chanjo hii kwa mwanamke mjamzito au mama anayenyonyesha. Lakini kuwa na mimba ama kunyonyesha sio sababu za kuepuka chanjo ya MenACWY. Mama mja mzito ama mwanamke. anayenyonyesha anatakiwa kupata chanjo hii kama yuko kwenye hatari ya kuambukizwa homa ya uti wa mgongo na ubongo.

Ikiwa una ugonjwa usio hatari kama vile homa, kuna uwezekano utapokea chanjo yako leo. Ikiwa wewe ni mgonjwa kiasi au sana, labda itakubidi usubiri hadi upone. Daktari wako anaweza kukushauri.

## 4 Hatari ya matukio ya chanjo

Unapotumia dawa zozote, hata chanjo, huwa kuna uwezekano wa madhara. Madhara haya huwa madogo na hupotea yenyewe baada ya siku chache, lakini mizio *(Alaji)* hatari pia inaweza kutokea.

Zaidi ya nusu ya watu wanaopokea chanjo ya homa ya uti wa mgongo ya ACWY huwa na matatizo yasiyo hatari baada ya kupokea chanjo, kama vile wekundu au maumivu katika sehemu ya sindano. Ikiwa matatizo haya yatatokea, kwa kawaida huisha baada ya siku 1 au 2.

Ni asilimia ndogo ya watu wanaopokea chanjo hii ambao hupata maumivu ya misuli au viungo.

**Matatizo yanayoweza kutokea baada ya kudungwa chanjo yoyote:**

- Wakati mwingine watu huzimia baada ya utaratibu wa matibabu, ikiwa ni pamoja na chanjo. Kuketi au kulala chini kwa dakika 15 kunaweza kusaidia kuzuia kuzirai na majeraha yanayosababishwa na kuanguka. Ni muhimu umwambie daktari wako ikiwa unahisi kizunguzungu, au kubadilika kwa namna unavyoona ama kama unasikia kelele katika masikio.
- Watu wengine hupata maumivu makali mabegani na huwa na ugumu wa kusongeza mkono mahali ambapo sindano ilidungwa. Jambo hili hufanyika mara chache sana.
- Dawa zozote zinaweza kusababisha mzio *(Alaji)* mkali. Mizio *(Alaji)* kama hii kutoka kwa chanjo huwa chache sana. Inakadiriwa takriban dozi moja kati ya dozi milioni moja, na inaweza kutokea kati ya dakika chache hadi saa chache baada ya kupata chanjo.

Kama dawa zozote zingine, kuna nafasi ndogo sana ya chanjo kusababisha majeraha makali au kifo.

Usalama wa chanjo hufuatiliwa wakati wote. Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti **www.cdc.gov/vaccinesafety**

## 5 Na kukiwa na mzio *(Alaji)* hatari?

**Ninafaa kutambua nini?**

- Ni muhimu kutambua kitu chochote kinachokutia wasiwasi, kama vile dalili za mzio mkali, homa kali sana, au tabia isiyo ya kawaida.

  Dalili za mzio mkali zinaweza kuchibua ngozi, uvimbe usoni na kwenye koo, ugumu wa kupumua, kasi ya mapigo ya moyo, kizunguzungu, na udhaifu kwa dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

**Ninafaa kufanya nini?**

- Ukidhani ni mzio *(Alaji)* mkali au ni jambo la dharura ambalo haliwezi kusubiri, piga simu 9-1-1 na uende katika hospitali iliyo karibu nawe. La sivyo, mpigie daktarin wako simu.

  Baadaye, unafaa kuripoti mzio huo kwenye "Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo" (VAERS). Daktari wako anafaa kutoa ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe kupitia tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov,** au kwa kupiga simu **1-800-822-7967.**

*VAERS huwa haitoi ushauri wa kimatibabu.*

## 6 Programu ya Taifa ya Kufidia Majeraha ya Chanjo

Programu ya kufidia Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa (VICP) ni programu ya shirikisho iliyoundwa kuwafidia watu ambao huenda wakawa wamejeruhiwa na chanjo fulani.

Watu wanaoamini wamejeruhiwa na chanjo wanaweza kupata maelezo kuhusu programu hii na kuhusu namna ya kuripoti madai kwa kupiga simu kupitia simu **1-800-338-2382** au kwa kutembelea tovuti ya VICP katika www.hrsa.gov/vaccinecompensation. Kuna kikomo cha muda wa kuripoti madai ya fidia (Malipo).

## 7 Ninawezaje kupata maelezo zaidi?

- Muulize mtoa huduma wako wa afya. Anaweza kukupatia kipeperushi cha furushi la chanjo au kupendekeza vyanzo vingine vya maelezo.
- Piga simu kwa idara ya afya iliyo karibu na wewe au ya jimbo lako.
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC):
  - Piga simu kwa **1-800-232-4636 (1-800-CDC-INFO)** au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika www.cdc.gov/vaccines

Kuwawezesha wahudumu wa afya kupata habari sahihi juu ya kinga maradhi, upimaji wa kinga maradhi, na ratiba iliyopendekezwa ya utoaji wa kinga maradhi hapo mbeleni, habari zitatumwa kwenye kituo cha Usajili wa uboreshaji huduma za Matibabu cha Michigan (Michigani Care Improvement Registry). Watu binafsi wana haki ya kuomba kwamba mhudumu wao wa afya asitume habari zinazohusu kinga maradhi kwenye kituo cha usajili.

Translation provided by the Minnesota Department of Health

Vaccine Information Statement (Interim)
Meningococcal ACWY Vaccines Kiswahili

Office use only

08/24/2018 | 42 U.S.C. § 300aa-26

DCH-0903SW AUTH: P. H. S., Act 42, Sect. 2126.